HOTUBA YA MHE. PROF. IBRAHIM HAMIS JUMA, JAJI MKUU WA TANZANIA KTIKA HAFLA YA UAPISHO WA NAIBU WASAJILI NA KUWAPATIA NYENZO ZA KAZI MAHAKIMU WAKAZI WAFAWIDHI WA MAHAKAMA ZA HAKIMU MKAZI

TAREHE 11.12.2023

Mhe. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi,

Mhe. Jaji Salma Maghimbi, Jaji Mfawidhi Kanda ya Dar es Salaam,

Wahe. Majaji Wafawidhi (Divisheni ya Ardhi, Divisheni ya Kazi, Divisheni ya Biashara, Kituo cha Usuluhishi, Kituo Jumuishi -Temeke, Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi),

Wahe. Majaji Mliopo,

Mhe. Dkt. Alex Malasusa, Askofu Mkuu wa KKKT,

Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama,

Mhe. Sylvester Kainda, Kaimu Msajili Mkuu wa Mahakama,

Mhe. Projestus Kahyoza, Kaimu Msajili wa Mahakama Kuu,

Leonard Magacha, Mtendaji Mahakama Kuu,

Marry Shirima, Mtendaji wa Mahakama Kuu Divisheni,

Naibu Wasajili Mliopo,

Watendaji wote wa Mahakama Mliopo,

Waheshimiwa Mahakimu,

Watumishi wote wa Mahakama Mliopo,

Wanahabari,

Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
Mahakama ya Tanzania!

1.0 PONGEZI KWA KUFIKA HATUA YA LEO BAADA YA MCHAKATO WA KUWAPATA NAIBU WASAJILI LEO HII

1.1 Kwanza nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kutujalia sote afya njema siku hii ya leo na kisha kuwapongeza Naibu Wasajili walioapishwa leo, hali kadhalika Mahakimu Wakazi Wafawidhi wa Mahakama za Hakimu Mkazi niowakabidhi nyenzo za kazi. Ni heshima kubwa kuaminiwa na kuteuliwa kushika nafasi za kiuongozi ya Naibu Wasajili na Mahakimu Wakazi.

1.2 Nafasi za Naibu Wasajili na Hakimu Wafawidhi, ni nafasi zenye umuhimu mkubwa katika uendeshaji na usimamizi wa shughuli za kimahakama. Mchakato wa kuwapata Naibu Wasajili hutumika pia kutambua watumishi wenye sifa, uwezo na maadili stahiki ya kuaminiwa na kupewa uongozi aidha kama Naibu Wasajili, Wakuu wa Idara, Vitengo na pia Mahakimu Wafawidhi.

1.3 Tume ya Utumishi wa Mahakama imepewa mamlaka chini ya Sheria ya Usimamizi wa Mahakama ya kuteua Naibu Wasajili kwa idadi itakayoona inafaa kwa kuzingatia majukumu yaliyopo na mahitaji ya siku zijazo.

1.4 Naibu Wasajili ni kada muhimu katika usimamizi wa masjala, ukaguzi na uendeshaji wa mashauri katika Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani. Hivyo basi, ni muhimu kuwa na idadi sahihi ya Naibu Wasajili ili kuimarisha utendaji katika maeneo hayo na hivyo kukidhi mahitaji ya utoaji haki nchini.

2.0 MCHAKATO WA MAPENDEKEZO YA MAJINA KWA AJILI YA KUFIKIRIWA KWA UTEUZI WA NAIBU WASAJILI

2.1 Tume ya Utumishi wa Mahakama kupitia Kamati Maalum ilipata jumla ya majina **485** kwa ajili ya kufanyiwa uchambuzi kwa makundi mbalimbali. Baada ya uchambuzi wa awali, Kamati iliamua kuwa jumla ya majina **345** ndiyo yafanyiwe uchambuzi hatua ya pili na Mahakimu **140** wasihusike kwenye mchakato awamu hii kwa sababu mbalimbali.

2.2 Usaili ndio ulitumiwa. Njia zilizotumika kuwapima ili kupata wanaoweza kufikiriwa kwa uteuzi wa Naibu Wasajili ni **usaili wa kuandika**, **kuhojiwa** pamoja **na tathmini ya hukumu zao, tabia na maadili**. Lengo hapa ni kupata Mahakimu bora zaidi kwa ajili ya kufikiriwa kwa uteuzi wa Naibu Wasajili, pia kuwa na Kanzi Data yenye majina ya wanaoweza kufikiriwa katika nafasi mbalimbali za uongozi wa Mahakama.

2.3 Mahakimu **40** ambao walikuwa tayari walishafanya usaili awamu iliyopita hawakufanya usaili wa kuandika bali waliakwa kwenye usaili wa kuhojiwa.

2.4 Mahakimu **130** walifanye usaili wa kuandika kwa njia ya mtandao.

2.5 Usaili uliisaidia Tume kujua uwezo wa wanaofikiriwa uteuzi. Aidha, usaili huo ulikusudia kuwapa wahusika fursa ya kushindania nafasi chache za Naibu Msajili na kuondoa dhana ya upendeleo kwenye uteuzi. Usaili uliwahusisha—Mahakimu Wakazi Wafawidhi wa Mikoa wapatao **sita (6)**; Mahakimu Wakazi Wafawidhi wa Wilaya **(110**), Mahakimu Wakazi Wakuu Daraja la II **wawili (2)**;

na Mahakimu Wakazi Waandamizi **kumi na mbili (12)**.

2.6 Kwa kuzingatia matokeo ya wasailiwa **130** waliofanya usaili wa kuandika kwa njia ya mtandao, jumla ya wasailiwa **86** waliitwa kwenye usaili wa kuhojiwa ana kwa ana.

2.7 Pamoja na usaili, vigezo vilivyozingatiwa na Tume katika kuwapata Naibu Wasajili vilikuwa— **Nidhamu na maadili**; **Uzoefu angalau zaidi ya miaka kumi akiwa Hakimu**; **Utendaji mzuri wenye matokeo yanayoonekana**; **Uwezo wa kueleza na kujieleza**; na **Uwezo kwenye uandishi wa hukumu**.

2.8 Ni vyema kuzingatia kuwa siyo wote ambao hawakuteuliwa walishindwa usaili ama hawakuwa na vigezo vinavyotakiwa, bali ni nafasi zilizotengwa na Tume ndio zilikuwa chache. Mtapitia kipindi cha Uangalizi Kazini *(Probation)* na ikigundulika kuwa wewe siye aliyetarajiwa, yapo majina ya kujaza nafasi zenu bila kupitia taratibu za Usaili.

2.9 Kuwahakikishia wale wote waliofanya vizuri na hawakupata uteuzi, majina yao yataendelea kuwa kwenye **Kanzi Data ya Tume** kwa kipindi fulani kadri Tume itakavyoona inafaa na endapo zitatokea nafasi nyingine wazi hivi karibuni, Tume haitalazimika kuendesha mchakato huu mrefu bali majina hayo ya kwenye hii Kanzi data yatafikiriwa.

2.10 Ujumbe kutoka Tume ya Utumishi wa Mahakama ni kuwa, nafasi za Uongozi unatokana ushindani na ulinganifu katika vigezo vya **Nidhamu** na **maadili**; **Uzoefu;** na **Uwezo**.

3.0 Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama Na. 4 ya Mwaka 2011 Imewekeza Matumaini Makubwa kwa Naibu Wasajili

3.1 Sheria ya Uendeshaji wa Mahakama imetumia lugha yenye kutoa uhuru mkubwa kwa Naibu Wasajili kutimiza majukumu yao bila kusubiri kuelekezwa au kupewa maagizo katika majukumu ambayo ni yao kisheria na kikanuni au kimazoea ya Kimahakama.

3.2 Sheria hii Namba 4 ya 2011, inatarajia viongozi katika nafasi za Naibu Wasajili na Mahakimu Wafawidhi wawe ni wale wanaojisukuma na kujituma wao wenyewe, wabunifu, wanatatua changamoto. Sheria Namba 4/2011 imewapa upeo wa kuona mbali, kutarajia matukio yajayo na kujitayarisha kwa tukio lolote katika kazi zao za kila siku.

3.3 Sheria Na.4/2011hii inapotamka kuwa, wewe Naibu Msajili, utakuwa ni msaidizi wa Msajili Mkuu, Msajili wa Mahakama ya Rufani au Msaidizi wa Msajili wa Mahakama Kuu katika kufanikisha usimamizi wa utekelezaji wa kazi za kimahakama *(to facilitate and supervise performance of the judicial functions)*, haitegemewi kila utakapokutana na jambo linalohitaji uamuzi wako, kwa mujibu wa sheria na kanuni utasubiri maagizo au maelekezo kutoka kwa viongozi hao unaowasaidia kutimiza wajibu wao.

4.0 Masjala za Mahakama ni Injini *(Engine Room)* ya Ufanisi na Weledi wa Mahakama

4.1 Sheria mbalimbali za Tanzania zimewapa Naibu Wasajili na Mahakimu Wafawidhi nafasi adhimu ya kusimamia shughuli za kila siku za kimahakama zinazopitia katika

masjala mtakazopangiwa kusimamia.

4.2 Masjala za Mahakama ni injini za Mahakama katika upatikanaji na utoaji haki. Mtu wa kwanza, ambaye mwananchi anayehitaji huduma za Mahakama atakutana naye, ni mtumishi katika mojawapo ya masjala inayoongozwa na Naibu Msajili au Hakimu Mfawidhi.

Katika kesi ya **Yusuph s/o Mbululo v. R,** Criminal Appeal No. 405 of 2018, mrufani alisubiri miaka 30 ili apatiwe nyaraka kutoka kwa Wasajili ili akate rufaa.

4.3 Chochote mtumishi atakachofanya au atakachoshindwa kufanya, kitahusishwa na ubora au udhaifu wa injini ya Mahakama chini ya usimamizi wa Naibu Msajili au Hakimu Mfawidhi. Kuongezeka au kushuka kwa imani ya wananchi kwa Mahakama kwa kiasi kikubwa itategemea ubora wa huduma kutoka katika masjala ya mahakama husika. Masjala ndio injini inayohusika na kupokea, kutuma na kuhifadhi nyaraka zote zinazosajiliwa kwa njia ya mtandao au kwa njia za usajili wa kawaida.

4.4 Masjala ndio sehemu ambayo Kanuni zilizotayarishwa na Kamati ya Kanuni ya Jaji Mkuu (Chief Justice's Rules Committee—JRC) hupitia ili kuleta mabadiliko na kufanya maboresho tarajiwa.

4.5 Masjala ndio Barabara kuu inayotiririsha taarifa za kimahakama baina ya ngazi mbalimbali za mahakama, wadau, mawakili na wale wote ambao watahitajika kuitikia wito wa kufika mahakamani au kufika katika masjala.

4.6 Hapana shaka yoyote kuwa, ufanisi wa Masjala unategemea sana aina ya Naibu Msajili au aina ya Hakimu Mfawidhi. Tume ya Utumishi wa Mahakama na Uongozi wa Mahakama utapenda kupata mrejesho kama nyie ni teuzi SAHIHI.

4.7 Nimeelezea awali namna Tume ya Utumishi wa Mahakama, hali kadhalika Uongozi wa Mahakama, zilivyotumia kila njia ili kuwapata nyie ikama Naibu Wasajili na Mahakimu Wafawidhi kwa matumaini kuwa mtasimamia Masjala kama injini bora ya utoaji wa Haki.

4.8 Watumiaji wa huduma zenu, watawapima, na watatoa mrejesho kuhusu ubora na ufanisi wa hizi injini mpya zilizofungwa katika masjala.

5.0 Ufanisi wa Masjala za Mahakama kama Injini ya Ufanisi na Weledi wa Mahakama Utategemea uongozi *(LEADERSHIP)* Usimamizi wa Watumishi katika Masjala husika

5.1 Naibu Msajili au Hakimu Mfawidhi ni viongozi wanaowasimamia watumishi wa kada mbalimbali walio chini yao ambao hutoa huduma zinazohusiana na utoaji haki. Nyie ni viongozi ambao majukumu yenu yanawaweka karibu na wadau muhimu wa Mahakama (Mawakili wa Serikali, Mawakili wa Kujitegemea, Magereza, Polisi, Ustawi wa Jamii) na kadhalika. Nyinyi ni Wasimamizi wakuu wa Watumishi wa Mahakama katika masjala na wale wanaohudhuria vikao vya mahakama kwa mfano Makarani wa Mahakama, Madalali wa Mahakama, Wasambaza Nyaraka. Kumbukeni kuwa Mapungufu katika ubora wa huduma za watumishi hawa hatimaye huchukuliwa kuwa ni mapungufu ya Naibu Msajili au Hakimu Mfawidhi anayewasimamia katika kazi zao za kila siku.

5.2 Haitatosha kwa Naibu Msajili au Hakimu Mfawidhi kufahamu Sheria zote kuhusu Mahakama, pamoja na miundo iliyopo, Kanuni, na Nyaraka zenye Miongozo ya kazi ndani ya Mhimili wa Mahakama bila kuonyesha matokeo chanya kutoka katika uongozi wako.

5.3 Wataalamu wa Maboresho wanatoa tahadhari adui mkubwa wa maboresho sio ukosefu wa rasilimali au mapungufu katika sheria, kanuni au taratibu zilizopo. Adui mkubwa wa maboresho ya Mahakama ni **tabia binafsi za watu**, **tamaduni,** na **mitazamo hasi zilizojificha chini ya barafu ya utumishi na utoaji huduma** *(underlying organisational culture that is not visible easily*). Kwa mafano Masjala yako inaweza kuwa ni injini ya utovu wa maadili. Uongozi ni kujua yale yaliyojificha na kuyarekebisha.

5.4 Yale yaliyojificha au kufichwa kama kucha, ndio muhimu wewe kiongozi lazima uyajue. Yaliyojificha na kufichwa kwako ndio hayo ambayo wananchi wanaotafuta huduma Mahakamani wanakutana nazo adha kama hizo kila siku Mahakamani. Baadhi ya tabia, mitizamo na tamaduni zilizofichwa chini ya barafu huonekana kwa wananchi kupitia kejeli, huduma isiyoridhisha na utovu wa maadili—kama—**lugha isiyo na**

heshima; **kuzungushwa kutafuta nakala za hukumu**, **mienendo ya mashauri kucheleweshа muda wa kukata rufani, barua kutojibiwa au kujibiwa kijumla jumla** (**tunashughulikia, mchakato unaendelea... utamu wa lugha ya Kiswahili utaiona pale unapopewa sababu ya kinachochelewesha huduma unayoitaka.**)

5.5 Tunapozungumzia Naibu Msajili au Hakimu Mfawidhi afanye maboresho ya mahakama, tunazungumzia pia kuzama chini na kutambua na kuondoa tabia, mitazamo hasi zilizojificha chini ya barafu ya utumishi na utoaji huduma.

5.6 Ni Wajibu wa Naibu Wasajili na Mahakimu Wafawidhi kupiga mbizi na kuzamia na kuwajua na kuwafahamu watumishi kwa tabia zao, mienendo na mitazamo ambayo haiendani na dhana ya maboresho. Fahamu pande mbili za watumishi (**CHANYA** na **HASI** ambazo hufichwa:

NEGATIVE- Unmotivated (Tabia Mbaya)	**POSITIVE- Motivated (Tabia Nzuri)**
<>Avoids taking initiative <> Defines his/her job description narrowly to avoid responsibility <> Does not take responsibility	<> Takes initiatives <> Comes with new and innovative, creative ideas <> flexible and ready to take up extra work.

<> Quick to blame others, to blame the law, to blame lack of finances <> procrastinates <> Gossipy (Ubuyu na Mbuyu)	<> Does not complain or blame others

NEGATIVE-Unethical/self interest (Tabia Mbaya)	**POSITIVE-Ethical (Tabia Nzuri)**
<>Disregards rules, procedures for his own benefits <> lacks commitment, cannot work without incentive, first to board the bus home <> produces shoddy works <> does not share information <>corrupt	<> respect rules, procedures, and goes out of his way to help others <> Very proud of his work and readily assists court users.

5.7 Katika Mafunzo elekezi, mtakumbushwa majukumu ya Naibu Wasajili na Mahakimu Wafawidhi pamoja na majukumu ya watumishi watakaotoa huduma chini ya usimamizi wenu.

5.8 Kila mmoja wenu lazima aifahamu ndani na nje ya masjala mtakazosimamia. Kwa mfano, kila shauri inalosajiliwa lina mtiririko wake maalum na hupitia vituo maalum hadi uamuzi kutolewa. Wewe kama kiongozi wa masjala ni lazima ufahamu kwa njia ya mtandao au kwa njia za kawaida, kuzifahamu mitiririko na vituo vyote ambazo mashauri mbali mbali hupitia, na endapo kuna mkwamo au ucheleweshwaji katika kituo chochote, mkwamuzi ni wewe.

6.0 UWEZO WA NAIBU WASAJILI NA MAHAKIMU WAFAWIDHI UTAPIMWA KILA SIKU KUPITIA MFUMO MPYA WA KURATIBU MASHAURI KWA NJIA ZA KI-ELEKTRONIKI (ELECTRONIC CASE MANAGEMENT SYSTEM—e-CMS)

6.1 MFUMO MPYA WA KURATIBU MASHAURI KWA NJIA ZA KI-ELEKTRONIKI tayari umeanza kufanya kazi kwa lengo la kuboresha huduma zinazolenga manufaa ya wananchi. Wengi wenu mmeshiriki kuujenga kupitia maoni na mapendekezo yenu.

6.2 Maboresho ya Mahakama kupitia huu mfumo mpya hautakuwa na maana kama mfumo mpya wa kuratibu mashauri utashindwa kusogeza haki karibu na wananchi na hauongezi viwango vya wananchi kuridhika na huduma za mahakama.

6.3 Naibu Wasajili na Mahakimu Wafawidhi nyinyi ndio injini ya MFUMO MPYA WA KURATIBU MASHAURI KWA NJIA ZA KI-ELEKTRONIKI (ELECTRONIC CASE MANAGEMENT SYSTEM—e-CMS)—

6.4 Wasajili na Wafawidhi nyie ndio mtawezesha Mfumo mpya wa kuratibu mashauri kwa njia za ki-elektroniki kurahisisha:

6.4.1-usajili wa mashauri kwa njia ya mtandao;

6.4.2-upangaji wa mashauri kwa Majaji na Mahakimu;

6.4.3-Uandishi wa hukumu na mienendo ya mashauri moja kwa moja kwenye mfumo tofauti na ilivyokuwa awali;

6.4.4– Vituo mbali mbali vya Mahakama kusomana na mifumo ya wadau wetu muhimu kama NIDA, NPS, RITA na kadhalika.

6.5 Uwekezaji mkubwa uliofanywa katika kujenga MFUMO MPYA WA KURATIBU MASHAURI KWA NJIA ZA KI-ELEKTRONIKI (ELECTRONIC CASE MANAGEMENT SYSTEM—e-CMS) utazaa matunda endapo Naibu Wasajili na Mahakimu Wafawidhi mtatekeleza wajibu wenu ipasavyo. Serikali iko katika safari ya kufikia utoaji wa huduma kwa njia za kidijitali – Tanzania ya Kidijitali.

7.0 NAIBU WASAJILI NA MAHAKIMU WAFAWIDHI MTAPIMWA KWA NAMNA MTAKAVYO SIMAMIA MPANGO WA KU-DIJITI NYARAKA ZOTE KATIKA MASJALA *(DIGITALIZATION OF COURT RECORDS)*

7.1 Timu ya wataalamu wa ndani ya Mahakama ambao walishirikiana na wataalam kutoka Mamlaka ya Serikali Mtandao *(eGA)* kutayarisha Mpango Kazi wa Kudijiti *('digitize')* nyaraka zote za mahakama katika masjala zote.

7.2 Naibu Wasajili na Mahakimu Wafawidhi nyinyi ndio mtakaoiwezesha Mahakama kubadili masjala zake kutoka mfumo wa analogi unaotegemea majalada magumu na makaratasi, hadi kuwa masjala ya kidijitali inayotumia mifumo ya kimtandao. Mkisimamia utekelezji wa Mpango Kazi mtaisaidia Mhimili wa Mahakama kusahau adha za upotevu wa nyaraka unaochangia ucheleweshwaji wa mashauri kukamilika. Mpango Kazi wa kidijitali utazaa matunda endapo mtatekeleza wajibu wenu vizuri ikiwemo kuainisha ukubwa, idadi ya kurasa na wingi wa nyaraka na majalada yaliyo katika kila Mahakama nchini zitakazotakiwa kufanyiwa *Digitization*.

8.0 UWEZO WA NAIBU WASAJILI NA MAHAKIMU WAFAWIDHI UTAPIMWA KWA KIASI GANI KANDA, DIVISHENI AU KITUO JUMUISHI KITAKAVYO TUMIA MATUNDA YA UWEKEZAJI MKUBWA ULIOFANYWA KUPITIA PROGRAMU YA UNUKUZI NA TAFSIRI *(TRANSCRIPTION & TRANSLATION—TTAJoTA)*

8.0 Mahakama ya Tanzania imedhamiria kufanya maborersho ambayo yatawaondolea Majaji na Mahakimu kuandika mienendo na kumbukumbu za mashauri kwa kutumia mkono. Leo hii, zama za AI huwezi kujenga hoja ya kuajiri stenographer kwa kila Jaji, Hakimu. Kampuni ya kimataifa kutoka Italy, ALMAWAVE ni moja ya makampuni bora duniani yanayojishughulisha na usukwaji wa mifumo inayotumia kufundisha mashine lugha kwa kutumia *Artificial Intelligence*, na katika uchanganuzi wa DATA *(leading company in AI, natural language analysis and BIG DATA solutions)*.

8.1 Mahakama ya Tanzania iliingia katika Makubaliano na ALMAWAVE ili kusuka mifumo ya unukuzi na kutafsiri mienendo ya mahakama kama sehemu ya programu ya maboresho ya mahakama inayotekelezwa na Serikali ya Tanzania kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia.

8.2 ALMAWAVE iliisuka na kuitengenezea Mahakama ya Tanzania mfumo wa kutambua sauti na papo hapo *(automatic transcription and translation)* kuiweka hiyo sauti katika maandishi ya lugha ya kiingereza au lugha ya Kiswahili kulingana na mahitaji ya mtumiaji.

8.3 Kwa maana nyingine, ALMAWAVE imeiweka Mahakama ya Tanzania katika Hali Bora ya kimaboresho yenye utayari kuhama kutoka kunakili kumbukumbu za Mahakama kwa mkono, hadi kubadili sauti na kuiweka katika maandishi ya lugha ya Kiswahili au Kiingereza. Kuhama huku, kutaharakisha utayarishaji wa kumbukumbu kwa mkono uliokuwa na hatari ya kuwa na makosa. Nugzo ya Pili- utoaji na upatikanaji wa Haki kwa Wakati.

8.4 Hizi mashini za kunakili na kutafsiri zinatakiwa zifungwe kwa awamu mbalimbali katika Mahakama zote **169** na kwa idadi sawa na vyumba vya mahakama zilizopo.

8.5 Katika awamu ya kwanza, vifaa vya kurekodi mashauri zimefungwa kwenye mahakama **kumi na moja (11)** na tayari majaribio ya matumizi ya vifaa hivyo yalifanyika. Kwa wakati huu, Naibu Wasajili na Mahakimu Wafawidhi nyinyi ndio sababu ya vifaa kunakili na kutafsiri kufanikiwa au kushindwa.

8.6 Seti hizo **kumi na moja (11)** zimeanza kutumika katika: Vituo Jumuishi **(Temeke, Kinondoni, Mwanza, Morogoro, Arusha** na **Dodoma)**; Mahakama Kuu **(Kanda ya DSM, Musoma, na Bukoba)**; na Divisheni za Mahakama Kuu **(Biashara na**

Uhujumu Uchumi). Wasajili na Mahakimu Wafawidhi nyinyi ndio wenye dhamana ya kuhakikisha vifaa vilivyofungwa na zile zitakazofungwa katika awamu zitakazofuata kweli zinatumika na pia zitatumika kwa faida kubwa ya kuboresha utoaji wa haki kwa wakati.

8.7 Ni nyie Naibu Wasajili na Mahakimu Wafawidhi ndio mtaiwezesha Mahakama ya Tanzania ivune faida kubwa ambayo Kampuni ya ALMAWAVE ya Italy imetaja:

8.7.1-Make the judicial process management efficient, fast, transparent and sustainable. [kufanya mchakato na mtiririko ya utoaji haki kwa ufanisi, haraka, uwazi na Endelevu].

8.7.2-Efficiency of the governance systems of African public sector bodies in which the technological expertise can play a leading role.[Ni sehemu ya ujezi wa utawala bora katika sekta ya Umma inayowezeshwa na teknolojia bora].

8.7.3-*Thanks to digitalization and Artificial Intelligence, judiciaries can manifest efficiency and reliability that benefits all stakeholders and help improve the business climate of Tanzania. [Kwa kuwekeza katika kudijiti na Akili Bandia, Mahakama zinakuwa na nafasi ya kuonyesha ufanisi, kuaminika mambo ambayo ni*

kwa manufaa ya wadau wote na pia inasaidia mazingira ya Biashara Tanzania].

9.0 MAFUNZO ELEKEZI

9.1 Najua mtapatiwa Mafunzo Elekezi. Jambo moja muhimu ambalo litajitokeza katika Mafunzo haya Elekezi, ni dhamira dhahiri ya Mahakama ya Tanzania kuwaingiza kuwa sehemu ya WABORESHAJI wa huduma za utoaji haki kupitia Mipango Mkakati na Programu za Maboresho.

9.2 Maboresho ya Mahakama yanayoendelea hivi sasa, yana lengo kuu la kujengautamaduni mpya, mitazamo mipya na mwelekeo mpya katika utoaji wa huduma za haki kwa kumlenga na kumridhisha mwananchi (*CITIZEN-CENTRIC JUDICIAL MODERNIZATION AND JUSTICE SERVICE DELIVERY).* Ninawasihi, muendelee kuwa sehemu ya dhana hii ya utoaji wa huduma za haki kwa kumlenga na kumridhisha mwananchi.

MWISHO

Baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Tume ya Utumishi wa Mahakama na Uongozi wa Mahakama ya Tasnzania, ninawatakia mafanikio makubwa katika nafasi zenu mpya.

AHSANTENI KWA KUNISIKILIZA